# MKATABA WA UCHIMBAJI MADINI.

**MKATABA HUU** umeandikwa na kusainiwa leo tarehe ...30... mwezi wa ...02..., 2024

**KATI YA**

**MASHAKA LUCAS MAJI,** mtu mzima wa sanduku la posta 85, Geita, (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**Mwenye Leseni**" tafasiri ambayo pale inaporuhusu itajumuisha wawakilishi ama warithi wake) kwa upande wa kwanza;

**NA**

**GOLDEN SUPPORT LIMITED,** kampuni yenye ukomo wa hatia yenye namba ya usajili **174300690** ambayo imesajiliwa nchini Tanzania chini ya sheria ya makampuni ya mwaka 2002 sura ya 212 (**the Companies Act, 2002 (Cap. 212)** ya sanduku la posta 72838, Dar es Salaam, Tanzania (ambayo katika mkataba huu itajulikana kama "**Kampuni ya uchimbaji**" tafasiri ambayo itahusisha pale inaporuhusu wawakilishi, wasimamizi ama warithi wake) kwa upande mwingine.

**UTANGULIZI:**

A. **AMBAPO** Mwenye Leseni ni mtu mzima anayemiliki leseni ndogo za uchimbaji madini (Primary Mining Licenses) namba **PML1627GTA, PML1626GTA, PML0899GTA, PML0897GTA, PML1784GTA na PML1785GTA,** na amehiari kuingia katika mkataba huu na Kampuni ya Uchimbaji ili kufanya shughuli za uchimbaji Dhahabu katika eneo la leseni tajwa zilizopo Nyamlilima - Geita, QDS 32/3 linalotambulika zaidi kwa co-ordinates (Arc 1960) ambazo zimeainishwa kwenye leseni tajwa na copi za leseni hizo zimeambatanishwa kwenye makataba huu.

B. **NA AMBAPO,** Mwenye leseni amejiridhisha kwamba Kampuni ya Uchimbaji imesajiliwa kihalali kufanya kazi za uchimbaji madini hapa nchini Tanzania na kwamba ina uwezo na utaalamu wa kiufundi anaouhitaji kufanya kazi zilizokusudiwa ndani ya leseni tajwa.

C. **NA AMBAPO** kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 8 cha sheria ya madini sura ya 123 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 (the **MINING ACT CAP 123 R.E 2019)** pande zote za makataba huu zimekubaliana kuunganisha na kubadili leseni ndogo zote sita (6) zilizotajwa (Primary Mining License) kuwa leseni kubwa (Mining License) ili kutimiza matakwa hayo ya sheria tajwa kwa lengo la kufanya shughuli za uchimbaji madini, kutengeneza faida, kuongeza thamani, kuwapa ujuzi wazawa, kupeana maarifa na utaalamu.

**HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO:-**

**SURA YA 1**

**1.0 TAFASIRI**

1.1 Katika mkataba huu maneno yafuatayo yatakuwa na tafasiri ifuatayo;

GOLDEN SUPPORT LIMITED REG. No: 174300690 TANZANIA P.O. Box 72838, DSM

"Mkataba" maana yake ni mkataba huu wa uchimbaji madini baina ya Mwenye Leseni na Kampuni ya Uchimbaji kwenye leseni ndogo za uchimbaji madini namba PML1627GTA, PML1626GTA, PML0899GTA, PML0897GTA, PML1784GTA na PML1785GTA;

"Leseni" maana yake ni leseni ndogo za uchimbaji madini namba PML1627GTA, PML1626GTA, PML0899GTA, PML0897GTA, PML1784GTA na PML1785GTA na pia itahusisha pia leseni ya kati ya uchimbaji madini (Mining License) inayotarajiwa kuombwa na wahusika wa mkataba huu;

"Wahusika" maana yake ni wale waliosaini mkataba huu;

"Vifaa" maana yake ni mitambo, mashine, vipuli, na vitu vyote vinavyomilikiwa, vilivyokodiwa au kuletwa katika mradi na Kampuni ya Uchimbaji.

"Eneo la Uchimbaji" maana yake ni eneo lote ndani ya leseni tajwa.

1.2 Marejeo ya nafsi ya umoja itahusisha, pale inapobidi, marejeo ya nafsi ya uwingi na kinyume chake.

1.3 Neno lenye kuelezea jinsia ya kiume litahusisha jinsia ya kike na kinyume chake. Pia neno lenye kuelezea utu litahusisha maana ya kampuni.

1.4 Vichwa vya habari vilivyotumika katika mkataba huu vitakuwa kwa ajili marejeo na tafasiri tu na havitaharibu maana halisi iliyokusudiwa katika masharti ya mkataba huu.

## SURA YA 2.

## 2.0 SHUGHULI ZA UCHIMBAJI MADINI.

2.1 Shughuli zote za uchimbaji madini zilizopo chini ya mkataba huu zitakuwa zinawahusu wahusika wote wa mkataba huu lakini Mwenye leseni hatahusika na gharama zozote za uendeshaji. Wahusika wa mkataba huu wamekubaliana kwamba Kampuni ya Uchimbaji itafanya kazi zote za uchimbaji na uchenjuaji madini pamoja na kufanya mambo mengine yote yanayohusiana na shughuli hizo kama vile kufanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa mradi, kununua kemikali za uchimbaji na uchenjuaji madini, kununua milipuko, kulipa gharama za uendeshaji wa mradi kama vile mishahara ya watumishi, ununuzi wa mafuta, ununuzi wa umeme, ulipaji wa bili za maji, ununuaji wa mahitaji ya chakula, ulipiaji wa vibali, ulipiaji wa ada za mwaka za leseni, kulipia gharama za uunganishaji na ubadilishaji wa leseni ndogo zilizotajwa kuwa leseni ya kati (Mining License), kulipa ada na ushuru wa serikali za mitaa au tozo zile zinazotozwa kwenye sheria, n.k. **na kwamba gharama hizo zitalipwa na Kampuni ya Uchimbaji na hazitakatwa wakati wa kugawana mapato**. Mapato ya yototе ya uzalishaji hayatakatwa gharama yoyote ile na yatagawanywa kwa mujibu wa kipengele cha 4.1 cha mkataba huu bila makato.

2.2 Leseni zote yaani **PML1627GTA, PML1626GTA, PML0899GTA, PML0897GTA, PML1784GTA** na **PML1785GTA** zinazomilikiwa na Mwenye Leseni zitabadilishwa kutoka kuwa leseni ndogo na kuwa Leseni ya kati (Mining License) na punde tu baada ya



SUPPORT LIMITED
REG No: 14300690
TANZANIA
P.O.Box 72838 DSM

kubadilishwa leseni hizo kuwa leseni ya kati (Mining License), leseni hiyo kubwa itahamishwa kwenda kwenye umiliki wa Kampuni ya Uchimbaji, ili iwe na jina la kampuni hiyo kabla ya shughuli za uchimbaji madini kuanza.

2.3 Shughuli za uchimbaji madini zilizotajwa katika mkataba huu zinaweza kuanza mara tu baada ya leseni ndogo tajwa kubadilishwa kuwa leseni ya kati (Mining License). Wahusika wa mkataba huu wamekubaliana pia kwamba shughuli za uchimbaji madini ndani ya leseni zitaanza kwa kuleta vifaa vya uchimbaji ndani ya miezi sita (6) kuanzia siku ya kupatikana leseni ya kati (Mining License).

2.4 Wahusika wote wa mkataba huu wamekubaliana kwamba kwa muda wote wa mkataba huu hakuna mtu mwingine yeyote yule (mzawa au raia wa kigeni) atakayeruhusiwa kuingia na kufanya shughuli za uchimbaji madini ndani ya leseni tajwa isipokuwa Kampuni ya Uchimbaji twajwa tu

2.5 Kampuni ya Uchimbaji pamoja na wataalamu wake watafanya kazi za uchimbaji madini katika namna ile wanayoona wao kuwa inafaa kulingana na utaalamu walionao lakini kwa kuzingatia matakwa ya mkataba huu yanayowataka wafanye uzalishaji wenye tija na kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususani sheria ya madini sura ya 123 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 pamoja na marejeo mengine ya sheria hiyo yatakayofanyika na kanuni zake.

2.6 Kampuni ya Uchimbaji italeta na kusimika mtambo wa kuchenjua madini **(CIP PLANT)** wenye thamani kati ya **USD 350,000** hadi **USD 450,000**. Kampuni ya Uchimbaji pia italeta na kusimika vifaa vingine vinavyotakiwa katika shughuli za uchimbaji tajwa. Gharama za ununuzi wa vifaa vya uchimbaji na gharama zote za uwekezaji hazitakatwa wakati wa kugawana mapato yanayotakiwa kugawanywa kwa mujibu wa kifungu cha 4.1. Mwenye Leseni hatawajibika na gharama za ununuaji wa vifaa vya uchimbaji.

2.7 Vifaa vyote vya uchimbaji vinavyomilikiwa na Kampuni ya Uchimbaji na kutumika kwenye shughuli za uchimbaji baada ya mgodi kufungwa vifaa hivyo vitabaki kuwa mali ya Kampuni ya Uchimbaji.

2.8 Kemikali zote, magazine na milipuko kama vile ammonium, detonators, IDF, n.k vitanunuliwa kutokana na chaguo la Kampuni ya Uchimbaji ili kampuni hiyo iweze kupata bidhaa bora zinazoendana na aina yake ya uchimbaji kwa bei nzuri.

2.9 Wahusika wa mkataba huu wakati wote wa uhai wa mkataba watahuisha leseni zao ziwe hai kwa ajili ya mradi na hawatazikopea ama kuzihusisha na mikopo, madai, pango au mazuio yoyote yale ya kisheria.

2.10 Wahusika wote wa mkataba huu watahusika na mahusiano ya kijamii na watawajibika kwa jamii (corporate social responsibility) kuhusiana na mradi wao.

GOLDEN SUPPORT LIMITED
REG. No. 174300690
TANZANIA

2.11 Wahusika wa mkataba huu watakuwa wanakutana kila baada ya miezi sita (6) kuangalia na kujadili mwenendo wa kazi zao na utekelezaji wa matakwa ya mkataba huu.

2.12 Uoto wa asili wote na majengo yasiyohamishika (fixtures) vitakavyokuwepo ndani ya leseni baada ya kumalizika kwa shughuli za uchimbaji madini ndani ya leseni (Isipokuwa vifaa vya uchimbaji vya Kampuni ya Uchimbaji) vitakuwa mali ya wahusika wote na asilimia za umiliki wao utakuwa ni ule wa 20/80 kama mgao wao wa faida unavyoelezwa na kipengele cha 4.1 cha mkataba huu.

**SURA YA 3.**

**3.0 MUDA WA MKATABA HUU.**

3.1 Mkataba huu **utakuwa hai kwa muda wote wa uhai wa mgodi na kwa kutegemea uwepo wa mwamba/mawe ya dhahabu yanayoweza kuzalishwa. (Permanent term depending on the availability of ore)** na pia uhai wa mkataba huu utazingatia masharti mengine ya sheria ya madini (**MINING ACT CAP 123 R.E 2019)** na kanuni zake.

**SURA YA 4**

**4.0 MALIPO NA NAMNA YA KULIPWA.**

4.1 Wahusika wa mkataba huu wamekubaliana kwamba mawe ya dhahabu yote yaliyozalishwa kwenye shughuli tajwa za uchimbaji yatafanyiwa uchenjuaji kwenye mitambo ya uchenjuani iliyopo kwenye maeneo ya mradi. Baada ya kutoka kufanya uzalishaji elution Kampuni ya Kuchimba **itachukua 85% ya Dhahabu (final product) au fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya Dhahabu tajwa** (bila kukata gharama yoyote) ikiwa ni mgao wake wa mapato ya uzalishaji na Mwenye Leseni atachukua **15% ya Dhahabu (final product) au fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya Dhahabu tajwa** (bila kukata gharama yoyote) ikiwa ni mgao wake wa mapato ya uzalishaji.

4.2 Kama wahusika wa mkataba huu wataamua kuuza dhahabu iliyopatikana kabla ya kugawana mapato, watafanya tu hivyo baada ya kuuza Dhahabu hiyo kwa mnunuzi yeyote (any dealer) aliyewapa bei ya juu zaidi ya wengine kwenye soko la dhahabu au popote pale watakapoona inafaa kwao kuuza kwa ridhaa yao wote na pesa za mauzo tajwa zitalipwa punde tu baada ya mchakato wa kuuza dhahabu hiyo kukamilika mchakata ambao kukamilika baada ya upimaji na uthaminishaji wa dhahabu kufanywa na maafisa wa tume ya madini kwenye soko la dhahabu.

4.3 Rekodi zote za upimaji, uthaminishaji na uuzaji wa dhahabu pamoja na malipo ya kodi zitafanyika kwa kutumika majina ya Kampuni ya Uchimbaji na kila nakala ya nyaraka au risiti ya upimaji, uthaminishaji na uuzaji wa dhahabu pamoja na malipo ya kodi ya dhahabu tajwa atapewa Mwenye Leseni kwa ajili ya kumbukumbu zake na ushahidi wa malipo ya kodi ya dhahabu hiyo kwa upande wake.

GOLDEN SPORT LIMITED REG. No.: 174300690 TANZANIA P.O. Box 72838 DSM

4.4 Malipo ya kodi ya uzalishaji ya 2% yaliyolipwa na Kampuni ya Uchimbaji yatamaanisha kuwa yamelipwa pia na Mwenye Leseni kwa mujibu wa mkataba huu (Malipo ya pamoja ya kodi ya uzalishaji).

4.5 Wahusika wa mkataba huu wanawajibika kulipa malipo ya pamoja ya mrabaha (Royalty) na kodi za TRA kutokana na uzalishaji wao wa pamoja na kwamba malipo hayo yatakatwa kabla ya kugawana mapato baina yao. Mirabaha (Royalties) tajwa haitakuwa muhimu kukatwa kwenye pesa za mauzo kama itakuwa inatakiwa kulipwa na mnunuzi wa dhahabu hiyo (dealer) kwa kuzingatia utaratibu uliopo katika soko la madini kwa wakati huo. Utaratibu wenye manufaa ulipo soko la madini ndio utakaotumika katika mambo ya mirabaha (Royalties). Hakuna makato ya Mrabaha (Royaltys) yatakayofanyika pasipo uwepo wa nyaraka za tume ya Madini Tanzania zinazoainisha na kutaka mrabaha huo ulipwe.

4.6 Endapo Kampuni ya Uchimbaji itachimba na kupata vito vya thamani (**Gemstones**) ndani ya eneo la leseni tajwa, vito hivyo vya thamani (Gemstone) vitauzwa kwa mujibu wa sheria, kodi za mapato zitalipwa na wahusika wote kwa pamoja kisha pesa ya mapato itagawanywa kwa panze zote za mkataba huu 15% kwa Mwenye Leseni na 85% kwa Kampuni ya Uchimbaji kama mkataba unavyoainisha.

4.7 Malipo yote ya mapato ya Mwenye Leseni yatalipwa na Kampuni ya Uchimbaji kwa mujibu wa maelekezo ya maandishi ya Mwenye Leseni.

## SURA YA 5

### 5.0 USALAMA KAZINI.

5.1 Imekubaliwa na wahusika kuwa, Kampuni ya Uchimbaji ndio taasisi pekee itakayokuwa inafanya kazi za uchimbaji kwa kutoa msaada wa kiufundi ndani ya leseni. Mwenye Leseni atawaondoa watu wengine wote wanaofanya shuguli katika leseni tajwa hii ikiwa ni kutekeleza yafuatayo;-

a) Hakutokei muingiliano wa shuguli zinazofanywa na Kampuni ya Uchimbaji.
b) Kutekeleza kanuni za usalama mahala pa kazi.
c) Kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanatimia.

## SURA YA 6

### 6.0 USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA MRADI.

6.1 Ni wajibu wa Kampuni ya Uchimbaji kusimamia usafirishaji na uhifadhi wa mawe yaliyozalishwa na kuhifadhiwa katika maeneo ya kazi ili kuhakikisha kuwa haki za wahusika wa mkataba huu hazipotei. Mwenye Leseni ana haki ya kuwa na wawakilishi wake katika eneo la kazi ili kuona na kujiridhisha juu ya utaratibu wa kazi na haki za wahusika lakini wawakilishi hao hawatakuwa na mamlaka ya utendaji ama utawala juu ya shughuli hizo.

6.2 Usimamizi na utawala (Management) wa shughuli zote za uchimbaji madini ndani ya maduara ya chini ama ya wazi utafanywa na Kampuni ya Uchimbaji pekee. Kampuni ya Uchimbaji itazifanya kazi hizo na kuzisimamia kiutawala kupitia bodi yake ya usimamizi na utawala ambayo kwa mujibu wa mkataba huu matendo yake yataiwajibisha Kampuni ya Uchimbaji pekee pasipo kumhusisha Mwenye Leseni kwa mambo yote ya uchimbaji ndani ya mashimo.

6.3 Usimamizi na utawala wa wafanyakazi, eneo la kazi na kambi zote utakuwa chini ya Kampuni ya Uchimbaji. Mwenye Leseni ana haki ya kuwa na wawakilishi katika maeneo hayo ya kazi lakini wawakilishi hao hawatakuwa na mamlaka ya utendaji ama utawala juu ya wafanyakazi hao ama shughuli hizo.

6.4 Pamoja na matakwa ya kipengele cha 6.2 na 6.3 vya mkataba huu, wahusika wote wa mkataba huu wana wajibu wa kushirikiana na kuhakikisha kazi zilizokusudiwa zinafanyika kwa mafanikio.

**SURA YA 7.**

## 7.0. MAJUKUMU YA WAHUSIKA WA MKATABA HUU.

**7.1. Yafuatayo yatakuwa majukumu ya Mwenye Leseni:-**

a) Kuipatia Kampuni ya Uchimbaji nyaraka zote muhimu zinazohitajika ili zoezi la kuunganisha na kubadilisha leseni ndogo kuwa leseni ya Kati (Mining License) lifanyike na pia kushirikiana na Kampuni ya Uchimbaji kufanikisha shughuli zilizokusudiwa. Pia Mwenye Leseni ataisaidia Kampuni ya Uchimbaji kufanikisha upatikanaji wa vibali mbalimbali vya uchenjuaji madini, vibali vya kulipua, Vibali vya kutunza milipuko na vibali vya kununua na kusafirisha milipuko na kemikali.

b) Kulipa mishahara ya wawakilishi ama wasimamizi wake mwenyewe kwenye maeneo ya kazi (Kama wapo).

c) Kuhakikisha kuna Amani na utulivu baina yake na Kampuni ya Uchimbaji ama watu wengine.

**7.2. Yafuatayo yatakuwa majukumu ya Kampuni ya Uchimbaji:-**

a) Kufanya malipo ya pamoja na Mwenye Leseni ya Mrabaha (Royalty) pamoja na kodi itokanayo na uzalishaji wa pamoja wa madini kwa TRA (2%).

b) Kutoa fedha za uendeshaji wa shughuli za uchimbaji.

c) Kununua vifaa na mitambo yote muhimu kuwezesha uzalishaji na pia kuweka umeme na maji kweye eneo la mradi wa uchimbaji.

d) Kuleta na kuwalipa watumishi waliofuzu, kuweka mtaji wa kuendeshea kazi ili kuongeza uzalishaji wa mawe ya dhahabu kwa kiwango cha juu ikiwa ni pamoja na kulipa gaharama za uzalishaji, mishahara ya watumishi wazawa na wale wa kigeni, gaharama za kisheria, kodi na gharama zote za uendeshaji.

SOLDER SUPPORT LIMITED
REG No.: 74300690
TANZANIA
P.O. Box 72838, DSM

e) Kufanya maandalizi ya shughuli zilizokusudiwa ziweze kuanza kufanyika mapema baada tu ya kupata leseni ya kati (Mining License).
f) Kuwapatia watu wanaomwakilisha Mwenye Leseni taarifa muhimu za uzalishaji ili wajue kiwango sahihi cha uzalishaji kwa ajili ya uhakiki wa taarifa zao.
a) Kuendeleza shughuli za uzalishaji wenye tija ndani ya eneo la leseni

7.3. **Yafuatayo yatakuwa majukumu ya pande zote mbili za mkataba huu:-**

a) Kushughulikia maswala yote ya umiliki wa leseni.
b) Kulipa ada za kuhuisha leseni kutoka kwenye mapato ya uzalishaji.
c) Kulipa malipo ya pamoja ya Mrabaha (Royalty) na kodi za TRA (2%) zitokanazo na uzalishaji .
d) Kulipa malipo ya pamoja ya ushuru na tozo zingine za serikali zitokanazo na uzalishaji kama vile Service Levy.
e) Kufanya mauzo ya dhahabu (Kama itakubaliwa na pande zote) kwa kutumika Taratibu za tume ya Madini Tanzania.
f) Kulipa kodi zingine za serikali na ushuru uliopo kisheria kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa sheria za kodi (Income Tax Act CAP: 332 R.E 2019) na kwa mujibu wa makadirio halali yatakayofanywa na maafisa wa TRA kwa wahusika wanaouza dhahabu. Kila upande utalipa kodi na ushuru ipasavyo.
g) Kushughulikia masuala ya mahusiano ya jamii.
h) Kushughulikia na kutekeleza masuala yote ya kimazingira yaliyoorodheshwa katika tathmini ya mazingira iliyofanywa kwenye mradi na wahusika wa mkataba huu. Wahusika wa mkataba huu watatekeleza utunzaji wa mazingira kama jinsi ulivyotathminiwa na mambo mengine yatakayoelekezwa na mamlaka za nchi.

## SURA YA 8

## 8.0 TAARIFA

8.1 Kutakuwa na notisi ya siku 90 kwa jambo lolote la ukiukwaji wa masharti ya mkataba huu litakalowasilishwa kwa upande uliokiuka kwa lengo la kutaka upande uliokiuka urekebishe ukiukwaji huo.

8.2 Endapo ukiukwaji huo hautarekebishwa na upande uliokiuka ndani ya siku 90 za notisi, basi ukiukwaji huo utakuwa ni ukiukwaji wa mkataba na upande unaoathirika na ukiukwaji huo unaweza kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na hatua zile zilizotajwa kwenye kipengele cha 9 na 10 cha mkataba huu.

8.3 Kwa minajiri ya taarifa kutoka upande mmoja kwenda mwingine wa mkataba huu, zifuatazo ni anuani zitakazotumika kufikisha taarifa baina ya pande husika;

...EN SUPPORT LIMITED REG. No: 174300690 TANZANIA P.O. Box 72838 ,DSM

**MWENYE LESENI:**

**MASHAKA LUCAS MAJI**
P.O. Box 81- Geita,
PHONE: 0784455754,

**KAMPUNI YA UCHIMBAJI:**

**GOLDEN SUPPORT LIMITED**
For the attention of MOHAMMED OTHMAN MOHAMMED MOHAMMED,
P.O. Box 72838, Dar es Salaam
PHONE: 0762507508
EMAIL: mohammedaljaf980@gmail.com

**SURA YA 9**

**9.0 UTATUZI WA MOGOGORO**

9.1 Mgogoro wowote utakaojitokeza baina ya wahusika juu ya mkataba huu utatatuliwa kwa njia ya usuluhishi baina ya wahusika kwa kushirikisha Tume ya Madini Tanzania ndani ya mwezi mmoja (1) baada ya kupeana taarifa ya mgogoro huo na endapo mgogoro huo utashindwa kutatuliwa basi mgogoro huo utapelekwa kwenye mahakama za Tanzania zenye mamlaka ya kuutatua.

**SURA YA 10**

**10.0 KUSITISHA MKATABA.**

10.1.1 Usitishaji wa mkataba huu unaweza kufanyika endapo yatatokea mambo yafuatayo:-

a) Kutokea ukiukwaji wa mkataba na kwamba ukiukwaji huo umeshindwa kurekebishwa ndani ya siku 90 baada ya taarifa ya maandishi kutolewa.

b) Baada ya kutokea matendo ya Mungu yanayoathiri pakubwa shughuli zilizokusudiwa (Force Majeure). Wahusika wa mkataba huu watachukua hatua stahiki kurekebisha matendo hayo ya Mungu kwa njia zote zilizopo na endapo itashindikana basi uvunjaji wa makatab uwe ndo suluhisho la mwisho.

c) Baada ya shughuli za uchimbaji kumalizika.

d) Mabadiliko ya sheria yanayoathiri mkataba huu na kuufanya usitekelezeka.

e) Kufilisika kwa wahusika wa mkataba huu.

f) Kama uzalishaji wa mawe ya dhahabu (ore) utaisha ama kupungua kwa kiasi kwamba haiwezi kufanya shughuli za uchimbaji kutekelezeka pasipo kuleta hasara na kwa mantiki hiyo ni muhimu mkataba huu kuvunjwa ili kuepusha hasara ya faida na mtaji kwa wahusika.



CamScanner

g) Kama mhusika yeyote ataamua kuvunja mkataba huu kwa sababu isiyo ya msingi na iliyo nje ya mambo yaliyoainishwa katika kifungu hiki cha 10 cha mkataba, basi mhusika huyo atamlipa mhusika mwingine fidia kwa hasara itokanayo na kuvunjika kwa mkataba huu.

**SURA YA 11**

**11.0 FIDIA YA ARDHI.**

11.1 Mwenye Leseni anaahidi kwa Kampuni ya Uchimbaji kuwa anamiliki eneo la ardhi yote iliyopo ndani ya leseni hivyo kwa wakati huu hapatakuwa na fidia yoyote ya ardhi kwa mtu yeyote yule juu ya mkataba huu. Endapo kutakuwa na mtu mwenye madai halali ya umiliki wa ardhi iliyopo ndani ya eneo basi itakuwa ni wajibu wa Kampuni ya Uchimbaji kumlipa fidia ya ardhi mtu huyo na gharama hizo za fidia ilizolipa Kampuni ya Uchimbaji hazitakatwa wakati wa mgawanyo wa mapato kwa mujibu wa kipengele cha 4.1 cha mkataba huu.

**ARTICLE 12**

**12.0 MALIPO YA KIINGILIO (GOODWILL).**

12.1 Wahusika wa mkataba huu wamekubaliana kuwa Mwenye leseni atalipwa malipo ya kiingilio (Goodwill) jumla ya kiasi cha **USD 35,000**. Malipo hayo ya kiingilio (Goodwill) yatalipwa kwa awamu mbili (installments) **awamu ya kwanza ya malipo (1st Installment)** ya jumla ya **USD 10,000** italipwa kwenye akaunti ya Bank Account ya Mwenye Leseni baada ya leseni ndogo sita kubadilishwa na kuwa leseni ya kati (Mining License) na ambapo **awamu ya pili ya malipo** (**2nd Installment**) ya kiasi cha **USD 25,000** italipwa hapo baadae wakati mradi ukiendelea.

**SURA YA 13**

**13.0 MKATABA HUU.**

13.1 Mkataba huu umekamilika kwa wahusika juu ya maswala yote yaliyokusudiwa katika baina yao na hapatakuwa na ahadi ama makubaliano mengine tofauti na haya yaliyoandikwa katika amakataba huu;

13.2 Hakuna mkataba utakaobadilisha, kusitisha ama kurekebisha mkataba huu kwa mdomo. Wahusika wakitaka kufanya hivyo basi wafanye kwa njia ya maandishi na kusaini mabadiliko ama marekebisho hayo.

13.3 Kifungu chochote cha mkataba huu ambacho kitaonekana kubatilishwa na sheria yoyote basi kitakuwa batili pasipo kuathiri vifungu vingine halali vya mkataba huu.

GOLDEN SUPPORT LIMITED
REG. No: 174300690
TANZANIA
P.O. Box 72838 DSM

SURA YA 14

## 14.0. AHADI NA UTHIBITISHO WA MWENYE LESENI.

Mwenye leseni anaahidi yafuatayo;-

14.1.1 Kwamba anahaki, nguvu na mamlaka kamili ya kuingia mkataba huu bila kuwepo kizuizi chochote, deni, ama madai ya mtu mwingine yeyote;

14.1.2 Kwamba endapo ataombwa na Kampuni ya Uchimbaji, atafanya yote na kusaini ama kufanikisha upatikanaji wa nyaraka zote muhimu zitakazofanikisha kazi zilizokusudiwa;

14.1.3 Anahaki miliki ya leseni zilizotajwa na kwamba leseni hizo hazijawekwa rehani kwenye mkopo, hazina madeni, hazijakodishwa kwa watu wengine na hazina kipingamizi chochote kile ju ya kufanyika makubaliano haya;

14.1.4 Kwamba leseni hizi hazijaathirika kivyovyote vile ama kuhitajika kufutwa ama kuhamishwa kwa mtu mwingine na mamlaka za kiserikali;

14.1.5 Kwamba Mwenye Leseni ataondoa watu wengine wote wanaofanya kazi ndani ya leseni ili wapishe shughili zilizokusudiwa zifanyike pasipo kuwepo muingiliano ama migogoro.

SURA YA 15

## 15.0 AHADI NA UTHIBITISHO WA KAMPUNI YA UCHIMBAJI.

Kampuni ya Uchimbaji inaahidi na kuthibitisha yafuatayo

15.1.1 Kampuni ya Uchimbaji ina nguvu na uwezo kamili wa kuingia mkataba huu na kutekeleza makubaliano haya.

15.1.2 Kusainiwa kwa mkataba huu na utekelezaji wake umeidhinishwa na Kampuni ya Uchimbaji na hautasababisha ukiukwaji wa kanuni na muundo wa uongozi wa Kampuni hiyo.

SURA YA 16

## 16.0 MASHARTI YA JUMLA.

16.1 Kila mhusika atachukua hatua zote muhimu za utekelezaji na kusaini kwa nyakati tofauti nyaraka muhimu zinazohitajika na kufanya yale yote yaliyo muhimu kufanyika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

16.2 Wahusika watatunza siri na kutovujisha kwa mtu yeyote mambo yote yanayohusu mkataba huu isipokuwa tu pale watakapokuwa wamekubaliana wao kwa maandishi kufanya hivyo ama pale watakapokuwa wamehitajika kufanya hivyo kwa matakwa ya sheria.

16.3 Mkataba huu hauwezi kubadilishwa isipokuwa kwa njia ya maandishi tu na kwa kukubaliwa na kusainiwa na wahusika wote.

GOLDEN ... LIMITED REG. No: 174300690 TANZANIA P.O. Box 72838 DSM

16.4 Isipokuwa kwa hiari ya kughairi, kitendo cha mhusika kughairi kupokea haki yake yoyote iliyoainishwa katika mkataba huu haitamaanisha kughairi kuchukua haki zake zingine zozote.

16.5 Mambo yote ya mkataba huu yatasimamiwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

16.6 Mkataba huu utakuwa kwa Lughaya Kingereza na Kiswahili na utakuwa na nakala tatu (3) zote zikiwa halali.

**SURA YA 17**

**17.0 FIDIA**

17.1 Mhusika yeyote wa mkataba huu atamfidia mhusika mwingine kwa hasara yoyote atakayokuwa amemsababisha moja kwa moja au kinyume chake kutokana na kufanya au kutofanya jambo au kufanya uzembe yeye mwenyewe ama wawakilishi wake ama watu walio chini yake kwa amri yake ama kinyume chake ama kutotimiza masharti ya makataba huu.

**SURA YA 18**

**18.0 KUFUNGA SHUGULI ZA UCHIMBAJI.**

**18.1.1** Wahusika wamekubaliana kuwa, baada ya shuguli za uchimbaji madini kumalizika, wahusika wote kwa pamoja wataandaa mpango wa kufunga shughuli za uchimbaji na kuutekeleza kwa pamoja.

**KWA KUSHUHUDIA MKATABA HUU,** wahusika wameweka sahihi zao kushuhudia makubaliano haya leo hii na mwaka huu kama ifuatavyo:-

**UMESAINIWA** na **KUWASILISHWA** hapa Geita
na **MASHAKA LUCAS MAJI** ambaye namfahamu/
Ametambulishwa kwangu na ..............................
mbele yangu leo hii tarehe 30th mwezi wa 07 2024.

.................................... **MWENYE LESENI**

MASHAPALE JAWELLERS
P. O. BOX 81, GEITA
MOB. 0784455754

**MBELE YANGU:-**
Jina: Batholomew Muyangi
Sahihi: ..............................
Anuani: S.L.P 435, Geita
Wadhifa: **WAKILI.**

Batholomew Muyangi
P.O. Box 435 Geita
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

GOLDEN SUPPORT LIMITED
REG. No: 174300690
TANZANIA
P.O. Box 72838, DSM

**UMESAINIWA** na **KUWASILISHWA** hapa ...Geita...
na ...AZAM. B.MOHAMMED... ambaye namfahamu/
Ametambulishwa kwangu na ...
mbele yangu leo hii tarehe ...30... mwezi wa...07... 2024.

...............................
**SHAHIDI**

**MBELE YANGU:-**
Jina: ...Bartholomew Munyangi...

Sahihi: ...........................
Anuani: ...S.L.P 485, Geita...
Wadhifa: **WAKILI.**

**UMESAINIWA** na **KUWASILISHWA** hapa ..................
kwa niaba ya **GOLDEN SUPPORT LIMITED** leo hii tarehe
........................ mwezi ....................... 2024

...............................
**MHURI WA KAMPUNI**

1. Jina: Mohammed Othman

   Sahihi: ...........................
   Anuani: ...........................
   Wadhifa: ...........................

2. Jina: ...........................

   Sahihi: ...........................
   Anuani: ...........................
   Wadhifa: ...........................

GOLDEN SUPPORT LIMITED
REG. No.: 174300690
TANZANIA
P.O. BOX 12838 DSM